MAELEZO YA KWELI KWA WAPOKEAJI NA WATOA HUDUMA

IDHINI YA MATUMIZ I YA DHARURA (EUA) YA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH ILI KUZUIA UGONJWA WA VIRUSI VYA KORONA VYA 2019 (COVID-19) KWA WATU WALIO NA UMRI WA MIAKA 16 NA ZAIDI

Unapewa Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ili kuzuia Ugonjwa wa Virusi vya Korona vya 2019 (COVID-19) unaosababishwa na SARS-CoV-2. Maelezo Haya ya Kweli yana maelezo yanayokusaidia kuelewa hatari na manufaa ya Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech, ambayo unaweza kupokea kwa sababu kwa sasa kuna janga la
COVID-19.

Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ni chanjo na huenda ikakukuzuia usiambukizwe COVID-19. Hakuna chanjo ya kuzuia COVID-19 iliyoidhinishwa na Shirika la Kudhibiti Chakula na Dawa la Marekani (FDA).

Soma Maelezo haya ya Kweli kuhusu Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech. Ongea na mtoa chanjo ikiwa una maswali. Ni chaguo lako kupokea Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19 indungwa kama msururu wa dozi 2, kila baada ya wiki 3, kwenye misuli.

Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech huenda isimlinde kila mtu.

Maelezo Haya ya Kweli huenda yakawa yamesasishwa. Kwa Maelezo ya Kweli ya hivi majuzi, tafadhali angalia www.cvdvaccine.com.

UNACHOHITAJI KUJUA KABLA YA KUTUMIA CHANJO HII

COVID-19 NI NINI?
COVID-19 husababishwa na virusi vya korona vinavyoitwa SARS-CoV-2. Aina hii ya virusi vya korona haijawahi kuonekana hapo awali. Unaweza kuambukizwa COVID-19 kupitia kugusana na mtu mwingine ambaye ana virusi. Ni ugonjwa hasa wa kupumua ambao unaweza kuathiri viungo vingine. Watu walio na COVID-19 wamekuwa na dalili mbalimbali zilizoripotiwa, kuanzia dalili hafifu hadi ugonjwa mkali. Dalili zinaweza kuonekana siku 2 hadi siku 14 baada ya kuwa katika hatari ya kuambukizwa virusi. Dalili zinaweza kujumuisha: homa ya joto au baridi; kikohozi; kuishiwa na pumzi; uchovu; maumivu ya misuli au mwili; maumivu ya kichwa; upotezaji mpya wa kuhisi ladha au harufu; koo kavu; kufungana pua kutoa kamasi; kichefuchefu au kutapika; kuhara.

JE, CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH NI NINI?
Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ni chanjo isiyoidhinishwa ambayo inaweza kuzuia COVID-19. Hakuna chanjo iliyoidhinishwa na FDA ya kuzuia COVID-19.

FDA imeidhinisha utumiaji wa dharura wa Chanjo ya Moderna ya COVID-19 ili kuzuia COVID-19 kwa watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi chini ya Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA).

Kwa maelezo zaidi kuhusu EUA, angalia sehemu ya "**Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) ni nini?**" mwishoni mwa Maelezo haya ya Kweli.

JE, UNAPASWA KUSEMA NINI KWA MTOA HUDUMA WAKO WA CHANJO KABLA YA KUPATA CHANJO YA MODERNA YA COVID-19?
Mwambie mtoa huduma wako wa chanjo kuhusu hali zako zote za kiafya, ikijumuisha ikiwa:

- una mizio yoyote
- una homa ya joto
- una shida ya kutokwa na damu au unatumia vipunguzi vya damu
- una kinga dhaifu mwilini au unatumia dawa inayoathiri kinga mwilini
- una ujauzito au unapanga kuwa mjamzito
- unanyonyesha
- umepokea chanjo nyingine ya COVID-19

NI NANI ANAPASWA KUPOKEA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH?
FDA imeidhinisha matumizi ya dharura ya Chanjo ya Moderna ya COVID-19 kwa watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi.

NI NANI <u>HAPASWI</u> KUPOKEA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH?
Hupaswi kupokea Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ikiwa:

- ulikuwa na athari kali ya mzio baada ya dozi ya awali ya chanjo hii
- ulikuwa na athari kali ya mzio wa kiungo chochote cha chanjo hii.

JE, CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH COVID-19 INA VIUNGO VIPI?
Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer BioNTech inajumuisha viungo vifuatavyo: mRNA, lipidi ((4-hydroxybutyl)azanediyl)bis(hexane-6,1-diyl)bis(2-hexyldecanoate), 2 [(polyethilini glikoli) -2000] - N, N-ditetradecylacetamide, 1,2-Distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine, na kolesteroli), kloridi ya potasiamu, phosphate ya potasiamu monobasic, kloridi ya sodiamu, dibasic sodium phosphate dihydrate dihydrate, na sukrosi.

JE, CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH HUPEANWA VIPI?
Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech itatolewa kwako kama sindano kwenye misuli.

Msururu wa Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ni dozi 2 zinazotolewa kila baada ya wiki 3.

Ikiwa utapokea dozi moja ya Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech, unapaswa kupokea kipimo cha pili cha chanjo hiyo hiyo wiki 3 baadaye ili kumaliza msururu wa chanjo.

JE, CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH IMEWAHI KUTUMIKA HAPO AWALI?
Chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19 ni chanjo isiyoidhinishwa. Katika tafiti za kimatibabu, takriban watu 20,000 wenye umri wa miaka 16 na zaidi wamepokea angalau dozi1ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech COVID-19.

JE, MANUFAA YA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH COVID-19 NI YEPI?
Katika utafiti wa kimatibabu unaoendelea, Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 imeonyeshwa kuzuia COVID-19 baada ya dozi 2 zinazopeanwa kila baada ya wiki 3. Muda wa ulinzi dhidi ya COVID-19 haujulikani kwa sasa.

JE, HATARI ZA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH COVID-19 NI ZIPI?
Athari zisizokusudiwa ambazo zimeripotiwa za Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech zinajumuisha:

- maumivu katika eneo lililodungwa sindano
- uchovu
- maumivu ya kichwa
- maumivu ya misuli
- baridi
- maumivu ya misuli
- homa ya joto
- uvimbe katika eneo lililodungwa sindano
- wekundu katika eneo lililodungwa sindano
- kichefuchefu
- kutohisi vizuri
- limfu zilizo na uvimbe (lymphadenopathy)

Kuna uwezekano mdogo sana kwamba Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 inaweza kusababisha athari kali ya mzio. Athari kali ya mzio kwa kawaida inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa moja baada ya kupata dozi yaChanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech. Kwa sababu hii, mtoa huduma wako wa chanjo anaweza kukuuliza ukae mahali ambapo ulipokea chanjo yako kwa ufuatiliaji baada ya chanjo. Ishara za athari kali ya mzio zinaweza kujumuisha:

- Ugumu wa kupumua
- Uvimbe wa uso wako na koo
- Mapigo ya moyo yaliyo ya haraka
- Upele mbaya mwili mzima
- Kizunguzungu na udhaifu

Huenda hizi zikawa sio athari zote zinazowezekana za Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Athari kali na zisizotarajiwa zinaweza kutokea. Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech bado inachunguzwa katika tafiti za kimatibabu.

JE, NINAPASWA KUFANYA NINI KUHUSU ATHARI HIZI ZISIZOKUSUDIWA?
Ikiwa unapata athari kali ya mzio, pigia simu 9-1-1, au nenda kwenye hospitali iliyo karibu.

Piga simu kwa mtoa huduma wa chanjo au mtoa huduma wako wa afya ikiwa una athari yoyote inayokusumbua au isiyoisha.

Kamilisha na uwasilishe ripoti kwa VAERS mtandaoni katika https://vaers.hhs.gov/reportevent.html. Kwa usaidizi zaidi wa kuripoti kwa VAERS piga simu kwa 1-800-822-7967. Tafadhali ingiza "EUA ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19" katika mstari wa kwanza wa kisanduku #18 wa fomu ya ripoti.

Isitoshe, unaweza kuripoti madhara kwa Pfizer Inc. kupitia maelezo ya mawasiliano yaliyotolewa hapa chini.

Tovuti	Nambari ya faksi	Nambari ya simu
www.pfizersafetyreporting.com	(1-866-635-8337)	(1-800-438-1985)

Unaweza pia kupewa chaguo la kujiandikisha katika v-safe. V-safe ni zana mpya ya hiari inayotegemea simu mahiri inayotumia ujumbe mfupi na utafiti wa wavuti ili kuona watu ambao wamepewa chanjo ili kutambua athari zisizokusudiwa baada ya
chanjo ya COVID-19. V-safe huuliza maswali ambayo husaidia CDC kufuatilia usalama wa chanjo za COVID-19. V-safe pia hutoa vikumbusho vya dozi ya pili ikiwa inahitajika na ufuatiliaji wa moja kwa moja kwa njia ya simu wa CDC ikiwa washiriki wataripoti athari kubwa ya kiafya kufuatia chanjo ya COVID-19. Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kujisajili, tembelea: www.cdc.gov/vsafe.

NA IKIWA NITAAMUA KUTOPOKEA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH?
Ni chaguo lako kupokea Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech.Ni chaguo lako kupokea au kutopokea Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech. Ikiwa utaamua kutopokea chanjo, haitabadilisha huduma yako ya kawaida ya matibabu.

JE, KUNA CHAGUO ZINGINE ZINAZOPATIKANA ZA KUZUIA COVID-19 KANDO NA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH?
Hivi sasa, hakuna chanjo mbadala iliyoidhinishwa na FDA inayopatikana kuzuia COVID-19. Chanjo zingine za kuzuia COVID-19 zinaweza kupatikana chini ya Idhini ya Matumizi ya Dharura.

JE. NINAWEZA KUPOKEA CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH PAMOJA NA CHANJO ZINGINE?
Hakuna maelezo kuhusu utumiaji wa Chanjo ya Moderna ya COVID-19 na chanjo zingine.

JE, NA IKIWA NINA MIMBA AU NINANYONYESHA?
Ikiwa una ujauzito au unanyonyesha, jadili chaguo zako na mtoa huduma wako wa afya.

JE, CHANJO YA COVID-19 YA PFIZER-BIONTECH ITANIPA UGONJWA WA COVID-19?
Hapana. Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 haina SARS-CoV-2 na haiwezi kukuambukiza COVID-19.

HIFADHI KADI YAKO YA CHANJO
Unapopokea dozi yako ya kwanza, utapata kadi ya chanjo kukuonyesha wakati wa kurudi kupata dozi yako ya pili ya Chanjo ya Moderna ya COVID-19. Kumbuka kuleta kadi yako unaporudi.

MAELEZO YA ZIADA
Ikiwa una maswali, tembelea tovuti au piga nambari ya simu iliyopeanwa hapa chini.

Ili kupata Maelezo ya Kweli ya hivi majuzi, tafadhali tambaza msimbo wa QR uliotolewa hapa chini.

Tovuti ya kimataifa	Nambari ya simu
www.cvdvaccine.com	(1-877-829-2619) (1-877-VAX-CO19)

JE, NINAWEZAJE KUPATA MAELEZO ZAIDI?
- Uliza mtoa huduma ya chanjo
- Tembelea CDC katika https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/index.html.
- Tembelea FDA katika https://www.fda.gov/emergency-preparedness-and-response/mcm- legal-regulatory-and-policy-framework/emergency-use-authorization.
- Wasiliana na idara ya afya ya umma ya eneo lako au ya jimbo.

JE, MAELEZO YANGU YA CHANJO YATAREKODIWA WAPI?
Mtoa huduma ya chanjo anaweza kujumuisha maelezo yako ya chanjo katika Mfumo wa Maelezo ya Chanjo ya mamlaka (IIS) ya jimbo/eneo lako au mfumo mwingine ulioteuliwa. Hii itahakikisha kwamba unapokea chanjo sawa wakati unarudi kwa ajili ya dozi ya pili. Kwa maelezo zaidi kuhusu IIS, tembelea https://www.cdc.gov/vaccines/programs/iis/about.html92 chars.

JE, PROGRAMU YA KUKABILIANA NA FIDIA ZA MAJERAHA NI NINI?
Programu ya Kukabiliana na Fidia za Majeraha (CICP) ni mpango wa serikali kuu ambao huenda ukakusaidia kulipia gharama za matibabu na gharama zingine maalum za watu fulaniambao wamejeruhiwa vibaya na dawa au chanjo fulani, ikijumuisha chanjo hii. Kwa ujumla, dai lazima liwasilishwe kwa CICP ndani ya mwaka mmoja (1) tangu tarehe ya kupokea chanjo. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu programu hii, tembelea
www.hrsa.gov/cicp/ au piga simu kwa 1-855-266-2427.

JE, IDHINI YA MATUMIZI YA DHARURA (EUA) NI NINI?
FDA ya Marekani imefanya Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech ipatikane chini ya utaratibu wa ufikiaji wa dharura uitwao EUA. EUA inaungwa mkono na tamko la Katibu wa Afya na Huduma za Binadamu (HHS) kwamba hali zipo

za kuhalalisha utumiaji wa dharura wa dawa na bidhaa za kibaolojia wakati wa janga la COVID-19.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 haijakaguliwa kwa namna sawa na bidhaa iliyoidhinishwa au iliyopitishwa na FDA. FDA huenda ikatoa EUA wakati vigezo Fulani vimetimizwa, ambavyo vinajumuisha kwamba hakuna njia mbadala za kutosha, zilizoidhinishwa na zinazopatikana. Zaidi ya hayo, uamuzi wa FDA unategemea jumla ya ushahidi wa kisayansi unaopatikana na unaonyesha kuwa bidhaa inaweza kuwa nzuri kuzuia COVID-19 wakati wa janga la COVID-19 na kwamba manufaa yanayojulikana na yanayowezekana ya bidhaa huzidi hatari zinazojulikana inazowezekana za bidhaa. Vigezo hivi vyote lazima vitimizwe ili kuruhusu bidhaa itumike kwa matibabu ya wagonjwa wakati wa janga la COVID-19.

EUA ya Chanjo ya COVID-19 ya Pfizer-BioNTech inatumika kwa muda wa Tamko la EUA ya COVID-19 inayohalalisha utumiaji wa dharura wa bidhaa hizi, isipokuwa ikomeshwe au kubatilishwa (baada ya hapo bidhaa huenda zisiweze kutumiwa tena).

Imetengenezwa na
Pfizer Inc., New York, NY 10017

Imetengenezewa kwa ajili ya
BioNTech Manufacturing GmbH
An der Goldgrube 12
55131 Mainz, Germany

LAB-1451-1.1

Ilisasishwa: Desemba 2020